

**WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO
TAASISI YA SANAA NA UTAMADUNI BAGAMOYO
(TaSUBa)**



MAOMBI YA KUJIUNGA NA CHUO KWA MWAKA WA MASOMO 2019/2020

Mkuu wa Chuo- TaSUBa (Zamani Chuo cha Sanaa Bagamoyo) anakaribisha maombi ya kujiunga na Chuo kwa kozi za Astashahada (Cheti) na Stashahada (Diploma) katika fani zifuatazo;

- i. Sanaa za Maonyesho na Ufundi (Performing and Visual Arts) - Muziki, Ngoma, Uigizaji, Sarakasi, Ufundi wa Jukwaa (Stage Technology) na Sanaa za Ufundi (Fine Art).
- ii. Picha Jongevu (Film and TV Production) - Uchukuaji wa Video (Video Shooting), Kuhariri Video (Video Editing), Kuongoza Filamu (Film Directing) na Uandishi Miswada ya Filamu (Script Writing).
- iii. Uzalishaji wa Muziki na Sauti (Music and Sound Production) - Kurekodi Sauti (Sound Recording), Kurekodi Muziki (Music Recording), Uzalishaji wa Muziki (Music Production) na Usimamizi wa Studio (Studio Management).

1. CHETI MWAKA MMOJA (One year Certificate – NTA 4)

SIFA ZA KUJIUNGA

Mwombaji anatakiwa awe na sifa ifuatayo;

- Aliyemaliza kidato cha Nne (**FORM IV**) na kupata Ufaulu wa kuanzia “D” Nne (4).

2. STASHAHADA (Two year Diploma – NTA 6)

SIFA ZA KUJIUNGA

Mwombaji anatakiwa awe na sifa moja wapo kati ya hizi zifuatazo;

- Awe amehitimu kidato cha Sita (**FORM VI**) na kupata Ufaulu wa kuanzia Principal Pass Moja (1) na Subsidiary Moja (1).
- Awe amehitimu ngazi ya Astashahada (Cheti NTA 4) kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na NACTE.
- Awe amehitimu kozi ya Ualimu **Daraja la III A** na mwenye ufaulu wa kuanzia “D” Nne (4) katika matokeo ya kidato cha Nne (**FORM IV**)

MAELEZO MENGINE

- Maombi yote yatumwe moja kwa moja Chuoni kwa kujaza FOMU ya maombi ambayo inapatikana Chuoni Bagamoyo na kwenye tovuti ya Taasisi www.tasuba.ac.tz.
- Ada ya maombi ni **Tsh.10,000/=** na malipo haya yatafanyika kupitia **BENKI** AU kwa njia ya simu kupitia **M-PESA, TIGO PESA** na **AIRTEL MONEY**. Stakabadhi ya malipo (Receipt/Bank Pay Slip) itaambatanishwa pamoja na maombi ya kujiunga na Chuo.
- Kabla ya kufanya malipo kwa njia ya simu au Benki tafadhali piga simu kupata **CONTROL NUMBER** kupitia namba za simu; **0716072288, 0688489654, 0712596757** au **0763275517**.
- Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **31/08/2019**.
- Kwa mawasiliano zaidi tumia anwani zifuatazo; **MKUU WA CHUO, TaSUBa, S.L.P 32, BAGAMOYO**, AU Barua pepe application@tasuba.ac.tz AU kwa kupitia namba za simu; **+255 (0)23 2440032, 0763408792, 0655840405, 0713297626** au **0784394933**.